**HOTUBA YA MHESHIMIWA SAMIA SULUHU HASSAN, RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA, WAKATI WA KUPOKEA RIPOTI YA TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI KUHUSU UCHAGUZI MKUU WA MWAKA 2020**
**IKULU, DAR ES SALAAM, TAREHE 21 AGOSTI, 2021**

*Mheshimiwa Dkt. Philip Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;*

*Mheshimiwa Dkt. Hussein Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi;*

*Mheshimiwa Kassim Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;*

*Mheshimiwa Hemed Abdulla, Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar;*

*Mheshimiwa Tulia Ackson, Naibu Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;*

*Mheshimiwa Zubeir Ali Maulid, Spika wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar;*

*Mheshimiwa Prof. Ibrahim Juma, Jaji Mkuu wa Tanzania;*

*Mheshimiwa Omar Othman Makungu, Jaji Mkuu wa Zanzibar;*

*Mheshimiwa Jaji wa Rufaa (Mst.) Semistocles Kaijage, Mwenyekiti wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi;*

*Mheshimiwa Jaji (Mst.) Hamid Mahmoud, Mwenyekiti wa Tume ya Uchaguzi Zanzibar;*

*Mheshimiwa Jaji Francis Mutungi, Msajili wa Vyama vya Siasa;*

*Waheshimiwa Viongozi Wastaafu mliopo;*

*Waheshimiwa Mawaziri mliopo;*

*Mheshimiwa Amos Makalla, Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam;*

*Waheshimiwa Wajumbe wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi;*

*Waheshimiwa Viongozi wa Vyama vya siasa mliopo;*

*Wakuu wa Vyombo vya Ulinzi na Usalama;*

*Dkt. Wilson Mahera, Mkurugenzi wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi;*

*Ndugu Hamis Kona Hamis, Mkurugenzi wa Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar;*

*Waheshimiwa Mabalozi na Wawakilishi wa Taasisi za Kimataifa;*

*Wawakilishi wa Asasi za Kiraia na Viongozi wa Dini mliopo;*

*Wageni Waalikwa, Wana-Habari, Mabibi na Mabwana:*

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

Nianze kwa kumshukuru sana Mwenyezi Mungu aliyetujalia uhai na kutuwezesha kukutana hapa. Aidha, naupongeza Uongozi wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi, chini ya Mheshimiwa Jaji wa Rufaa (Mst.) Kaijage kwa kunishirikisha kwenye tukio hili la kupokea Ripoti ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020. Kimsingi, tukio hili sio la kisheria, bali ni utaratibu ama utamaduni uliowekwa na Tume yetu kwamba, kila baada ya Uchaguzi Mkuu, inaandaa Taarifa ama Ripoti na kuiwasilisha kwa Rais.

Malengo makuu ya utaratibu huu ni mawili. Kwanza, ni kuashiria kumalizika kwa zoezi la Uchaguzi Mkuu. Pili, ni kuiweka wazi Taarifa rasmi ya Uchaguzi Mkuu ili kutoa nafasi kwa wadau wa uchaguzi kuichambua na kuainisha mafanikio na changamoto zilizojitokeza; na hatimaye

kupendekeza namna ya kuboresha chaguzi zijazo. Kwa msingi huo, naipongeza Tume ya Taifa ya Uchaguzi kwa kubuni na kuendeleza utamaduni huu.

Nitumie fursa hii pia kuwashukuru Viongozi wa Serikali zetu mbili pamoja na wageni wetu waalikwa kwa kuhudhuria tukio hili. Kwa namna ya pekee, nawashukuru na kuwapongeza Viongozi wa Vyama vya Siasa mlioshiriki tukio hili. Uwepo wenu hapa leo sio tu unadhihirisha umuhimu wa tukio hili bali pia ni uthibitisho kuwa siasa sio uhasama. Ni kweli, kwenye Uchaguzi Mkuu uliopita CCM ilipata ushindi mkubwa, lakini hiyo haijawazuia kuhudhuria tukio hili. Ahsanteni sana kwa kuonesha ukomavu wenu mkubwa wa kisiasa.

***Waheshimiwa Viongozi, Wageni Waalikwa,***
***Mabibi na Mabwana;***

Uchaguzi ni zoezi muhimu katika nchi. Ni zoezi linaloashiria kukua na kukomaa kwa demokrasia katika nchi. Kupitia uchaguzi, wananchi hupata fursa ya kuwachagua viongozi wanaowataka kwa hiari; na kwa upande mwingine, Uchaguzi unawafanya viongozi waliochaguliwa kufanya kazi kwa kujiamini kwa kuwa wana ridhaa ya wananchi wanaowaongoza. Pamoja na ukweli huo, ili uchaguzi ukidhi malengo hayo ni lazima usimamiwe vizuri. Kinyume chake, Uchaguzi unaweza kuwa chanzo cha fujo na vurugu kama ambavyo imekuwa ikishuhudiwa kwenye baadhi ya nchi.

Ni kwa kuzingatia hayo, napenda kutumia fursa hii kutoa pongezi nyingi kwa Uongozi wa Tume yetu ya Taifa

ya Uchaguzi ikiongozwa na Mwenyekiti wake, Jaji wa Rufaa (Mst.) Kaijage, pamoja na Makamishna na Mkurugenzi wa Tume ya Uchaguzi, Dkt. Wilson Mahera, kwa kusimamia na kuendesha vizuri Uchaguzi wa mwaka jana. Hakuna shaka, kwa yeyote aliyeshiriki ama kushuhudia Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020 atakubaliana nami kuwa, Uchaguzi ulifanyika vizuri sana tena kwa kiwango cha juu kabisa.

Mwenyekiti wa Tume ametaja mambo yaliyofanyika kufanikisha Uchaguzi Mkuu wa Mwaka jana. Vifaa vilikuwepo vya kutosha na vilifika kwenye maeneo husika kwa wakati. Aidha, kwa mara ya kwanza kulikuwepo na karatasi maalum za kupigia kura kwa wenzetu wenye ulemavu wa kuona na hivyo kuwafanya wale wanaofahamu kuzitumia wapige kura bila kuhitaji usaidizi.

Zaidi ya hapo, kwenye Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020, idadi ya vituo vya kupigia kura iliongezwa hadi kufikia **81,567** kutoka vituo **65,105** mwaka 2015. Na hii ndiyo sababu wakati wa kupiga kura hapakuwepo na misururu mirefu. Vilevile, ili kuhamasisha wananchi wengi kupiga kura, Tume iliamua Uchaguzi huo ufanyike siku ya Jumatano na Serikali ikatangaza siku hiyo kuwa ya mapumziko. Kutokana na maandalizi mazuri ya Uchaguzi yaliyofanyika, matokeo yalitangazwa mapema, ndani ya saa **48**. Nawapongeza sana Tume ya Taifa ya Uchaguzi kwa kazi nzuri mliyoifanya.

Nawapongeza pia Watanzania kwa kushiriki kikamilifu kwenye Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020; kuanzia zoezi la kujiandikisha katika Daftari la Kudumu la

Wapiga Kura na kushiriki kwenye Kampeni. Zaidi ya hapo, nawapongeza wale waliotimiza Haki yao ya Kikatiba na kiraia ya kupiga kura. Kama tulivyosikia, jumla ya wapiga kura **15,091,950** walishiriki kupiga kura, sawa na **asilimia 50.72** ya wapiga kura **29,754,699** waliojiandikisha. Niwapongeze pia Watanzania kwa kuwezesha Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020 kugharamiwa na sisi wenyewe, ambapo kiasi cha **shilingi bilioni 416.8** kilitumika (**shilingi bilioni 154.3** kuboresha Daftari la Wapiga Kura na **shilingi bilioni 262.5** zoezi la Uchaguzi wenyewe). Hili ni jambo kubwa sana, ambalo naamini litaendelezwa.

Nawapongeza na kuwashukuru Viongozi wetu wa dini kwa kuliombea Taifa letu katika kipindi chote cha Uchaguzi. Navipongeza pia Vyombo vyetu vya Ulinzi na Usalama kwa

kusimama imara na hatimaye kufanikisha Uchaguzi wetu kumalizika kwa amani na usalama. Vilevile, navipongeza vyombo vya habari kwa kutoa taarifa na kuhamasisha wananchi kwenye zoezi la Uchaguzi. Nazipongeza Asasi za Kiraia zilizotoa elimu ya Mpiga Kura. Aidha, nawapongeza Watazamaji wote wa Uchaguzi. Nataka niwahakikishie kuwa ushauri wao tutautilia maanani.

Shukrani zangu pia ziende kwa Vyama vya Siasa pamoja na Wagombea wote walioshiriki kwenye Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020. Kwa namna ya pekee, nakipongeza Chama Cha Mapinduzi (CCM) kwa kupata ushindi mkubwa kwenye Uchaguzi Mkuu uliopita. Na kwa kuwa mimi ni Mwenyekiti wa CCM, napenda nitumie fursa hii pia kuwashukuru wanachama, wapenzi, washabiki na

wananchi wote waliotupigia kura kwenye Uchaguzi Mkuu uliopita. Aidha, tunawashukuru wale ambao hawakutupigia kura kwa kutekeleza haki yao ya kidemokrasia.

***Waheshimiwa Viongozi;***
***Wageni Waalikwa, Mabibi na Mabwana;***

Waswahili tuna usemi, *"Penye mafanikio changamoto hazikosekani"*. Hivyo basi, pamoja na mafanikio yaliyopatikana kwenye Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020, zilikuwepo baadhi ya changamoto. Na hii, kama nilivyosema, ndiyo moja ya sababu ya kuandaliwa kwa Ripoti hii na kuwekwa hadharani ili kutoa fursa kwa wadau wa uchaguzi na wananchi kuichambua na kuainisha mafanikio na changamoto; na hatimaye kutoa mapendekezo ya kuboresha chaguzi zijazo. Na katika hilo, nimefurahi sana kuona kuwa, kwenye Maelezo yaliyotolewa na Mwenyekiti

wa Tume hivi punde, ametaja baadhi ya mapendekezo yaliyotolewa na wadau mbalimbali yenye lengo la kuboresha chaguzi zetu zijazo.

Ametaja mapendekezo ya kuangalia uwezekano wa kuunganisha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343 na Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa, Sura ya 292. Yametolewa pia mapendekezo ya Uchaguzi Mkuu na Uchaguzi wa Serikali za Mitaa kusimamiwa na mamlaka moja. Vilevile, amezungumzia kuhusu uwezekano wa kuwa na watendaji wa Tume hadi kwenye Ngazi za Halmashauri na halikadhalika Serikali kuona uwezekano wa kutoa ruzuku kwa asasi za kiraia zinazotoa elimu ya mpiga kura katika hatua mbalimbali za mchakato wa uchaguzi.

Mapendekezo yote haya kimsingi ni mazuri na yanajadilika. Mathalan, suala la kuunganisha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343 na Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa, Sura ya 292 na kuzifanya chaguzi zote kusimamiwa na chombo kimoja ni jambo linalowezekana. Cha muhimu ni kwa wadau kukutana na kulijadili kwa kina pendekezo hilo kwa vile kila jambo lililoanzishwa lina msingi wake. Hata hivyo, ugumu nauona kidogo kwenye mapendekezo kuhusu ruzuku kwa Asasi za Kiraia na kuwa na watendaji wa Tume hadi kwenye ngazi ya Halmashauri. Mapendekezo haya yataongeza mzigo mkubwa kwa Serikali. Hata hivyo, yote hayo ni mambo yanayozungumzika, na yanaweza kufanyiwa kazi kwa kadri ya uwezo wa Serikali.

***Mheshimiwa Mwenyekiti wa Tume ya Uchaguzi;***
***Waheshimiwa Viongozi mliopo;***
***Wageni Waalikwa, Mabibi na Mabwana;***

Tupo hapa kwa ajili ya kushuhudia makabidhiano ya Taarifa ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020. Hivyo, haitakuwa busara kwangu kuwachosha kwa hotuba ndefu. Hata hivyo, kabla sijahitimisha hotuba yangu napenda niseme mambo machache ya mwisho.

Kwanza kabisa, ni kuhusu ushiriki wa wananchi kwenye uchaguzi. Nchi yetu ina idadi kubwa ya wanawake kuliko wanaume. Na hii inadhihirishwa na idadi ya waliojiandikisha kupiga kura mwaka jana. Kati ya wapiga kura **29,754,699** waliojiandikisha, **14,985,980** walikuwa wanawake (**asilimia 50.4**) na wanaume walikuwa **14,768,719** (**asilimia 49.6**). Nina uhakika, watu wengi waliojitokeza

kupiga kura pia walikuwa wanawake. Licha ya wingi huo, idadi ya wanawake waliojitokeza na kuteuliwa na Vyama vyao kuwania nafasi mbalimbali ilikuwa ndogo. Mwenyekiti wa Tume ametaja takwimu. Kati ya Wagombea **30** wa nafasi ya Urais na Wagombea Wenza, wanawake walikuwa **7** tu. Kwenye Ubunge, kati ya wagombea **1,257** wanawake walikuwa **293** na kwenye Udiwani wanawake walikuwa **668** kati ya wagombea **9,231**.

Hivyo basi, napenda kutumia fursa hii, kwanza, kuzihimiza Asasi za Kiraia kuendelea kutoa elimu na kuwahamasisha wanawake kuwania nafasi mbalimbali za Uongozi kwenye chaguzi zinazofanyika. Aidha, nawahimiza wanawake wenyewe kujiamini na kujitokeza kuwania nafasi mbalimbali za uongozi. Halikadhalika, natoa rai kwa Vyama

vya Siasa kuwaamini wanawake na kuwateua kuwania nafasi mbalimbali za uongozi. Nchi yetu haiwezi kupata maendeleo kwa haraka endapo zaidi ya nusu ya wananchi wake, ambao ni wanawake, watabaki nyuma. Ni watu wote washirikishwe ili twende pamoja.

Jambo la pili ni kuhusu matumizi ya TEHAMA. Dunia, kama ambavyo nimekuwa nikisema mara nyingi, ipo kwenye mapinduzi ya nne ya viwanda yanayoongozwa na TEHAMA. Shughuli nyingi duniani kwa sasa, ikiwemo masuala ya uchaguzi, yanafanyika kwa njia ya TEHAMA. Hivyo basi, nasi hatuna budi kujipanga katika mwelekeo huo kwa yale maeneo tunayoweza. Matumizi ya TEHAMA yatasaidia mambo mbalimbali, ikiwemo kuongeza idadi ya wapiga kura kwa sababu watu wengi wanashindwa kupiga

kura kwa vile utaratibu wa sasa unamlazimu mtu kupiga kura mahali alipojiandikisha. Uzoefu unaonesha kuwa kutokana na sababu mbalimbali baadhi ya watu wengi wanashindwa kupiga kura kwa vile siku ya kupiga kura wanakuwa nje ya vituo vyao. Kwa hiyo, tunaweza kuweka mfumo mzuri wa kuwawezesha watu wa namna hiyo kupiga kura mahali walipo.

Sambamba na hilo, hatuna budi kuziangalia Sheria zetu ili zisitumike kuwanyima watu haki kwa masuala ya kiufundi. Mathalan, mtu kuenguliwa kugombea kwa sababu tu ya kukosea kuandika baadhi ya herufi kwenye jina lake. Inawezekana tuweka utaratibu mzuri ili, badala ya kumwengua, mhusika aruhusiwe kurekebisha taarifa zake na hatimaye kuendelea kushiriki kwenye Uchaguzi. Lakini

hii haimanishi kuwa wagombea wasiwe makini katika kujaza fomu.

*Mabibi na Mabwana*, nihitimishe kwa kurudia tena kuwashukuru na kuwapongeza Tume kwa kukamilisha Ripoti ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020 na kunishirikisha kwenye Hafla hii. Ripoti yenu tumeipokea na tutaigawa kwa taasisi mbalimbali ili kupata maoni yao. Nawashukuru pia wageni wote waalikwa kwa kuhudhuria Tukio hili.

Nimefurahi kuona katika hafla hii tunao Viongozi kutoka Serikali ya Zanzibar wakiongozwa na Mhe. Rais wa Zanzibar, Dkt. Mwinyi, na Mwenyekiti wa Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar, Jaji Mstaafu Hamid Mahmoud. Serikali ya Zanzibar na Tume ya Uchaguzi Zanzibar ni wadau muhimu katika mchakato wa Uchaguzi. Hili

linathibitishwa na ibara ya 74 (13) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambayo inatamka kwamba ***"Katika kutekeleza majukumu yake, Tume ya Uchaguzi ya Jamhuri ya Muungano itashauriana mara kwa mara na Tume ya Uchaguzi ya Tanzania Zanzibar".***

Narudia kuwashukuru wadau wote walioshiriki kufanikisha Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020. Wito wangu kwa Tume ya Taifa ya Uchaguzi, mwisho wa Uchaguzi wa Mwaka 2020 ndiyo mwanzo wa maandalizi ya Uchaguzi wa Mwaka 2025. Hivyo, nendeni mkajipange ili Uchaguzi wa Mwaka 2025 ukawe bora na mzuri zaidi, kwa kuzingatia mapendekezo mbalimbali yatakayotolewa na wadau.

Baada ya Kusema hayo:

***Jamhuri ya Muungano wa Tanzania!***

*Mungu Zibariki Tume zetu mbili za Uchaguzi!*

*Mungu Ibariki Tanzania!*

**"AHSANTENI SANA KWA KUNISIKILIZA"**